JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2021

## URAIA NA MAADILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2021

# 06 URAIA NA MAADILI

*Kimechapishwa na*

Baraza la Mitihani la Tanzania,

S.L.P 2624,

Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI .......................................................................... 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI....... 2

2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha ........................... 2

2.1.1 Swali la 1. Kuwa Mwadilifu..................................................... 3

2.1.2 Swali la 2 : Kuheshimu Jamii .................................................. 9

2.1.3 Swali la 3: Kuithamini Jamii .................................................. 15

2.2 Sehemu B : Maswali ya Majibu Mafupi........................................ 22

2.2.1 Swali la 4: Kudumisha Amani ................................................ 22

2.2.2 Swali la 5 Kuwa Mstahimilivu................................................. 28

2.2.3 Swali la 6: Kuwa Mwajibikaji ................................................. 36

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI........................................................................ 43

4.0 HITIMISHO ............................................................................ 44

5.0 MAPENDEKEZO ..................................................................... 45

Kiambatisho ............................................................................... 47

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linayo furaha kutoa Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2021.

Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera na wadau wengine wa elimu kuhusu maarifa, stadi na ujuzi ambao wanafunzi waliweza kupata au kutopata katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Msingi. Hivyo, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu, unaweza kutumika kama kipimo cha ufanisi katika utekelezaji wa mtaala huo kwa lengo la kuboresha utoaji wa elimu inayowajengea wanafunzi uwezo katika umahiri mbalimbali wa somo la Uraia na Maadili.

Katika taarifa hii, dosari na mambo mbalimbali ambayo yamechangia wanafunzi kushindwa kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi yameainishwa ikiwa ni pamoja na kushindwa kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa mdogo wa umahiri mbalimbali, na kushindwa kuhawilisha maarifa. Aidha, chati ya ulinganifu wa ufaulu wa umahiri kwa mwaka 2020 na 2021 imewekwa kuonesha jinsi wanafunzi walivyofaulu katika kila umahiri uliopimwa katika miaka hii miwili.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa dosari zilizoainishwa katika taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi ili kuongeza ujuzi na maarifa ya wanafunzi.

Mwisho, Baraza linapenda kutoa shukrani za dhati kwa maafisa mitihani na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili ulifanyika tarehe 29 mwezi wa Oktoba mwaka 2021. Jumla ya wanafunzi 1,681,769 waliandikishwa kufanya upimaji huu ambapo wanafunzi 1,560,818 sawa na asilimia 92.81 walifanya upimaji huu. Aidha, ufaulu wa wanafunzi katika somo hili unaonesha kuwa wanafunzi 1,423,379**,** sawa na asilimia 91.20 walifaulu na wanafunzi 137,439 sawa na asilimia 8.8 hawakufaulu. Ufaulu huu umepungua ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo wanafunzi 1,702,775 (95.46%) walifaulu huku wanafunzi 77,370 (4.54%) hawakufaulu.

Upimaji ulikuwa na jumla ya maswali sita (6) yenye jumla ya vipengele 25, yaliyogawanyika katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali matatu (3) yenye jumla ya vipengele 13 vyenye jumla ya alama 26. Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) yenye jumla ya vipengele 12 vyenye jumla ya alama 24. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu zote A na B. Upimaji ulikuwa na jumla ya alama 50.

Katika sehemu A, wanafunzi walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika kwenye kisanduku, kuoanisha maelezo kuhusu alama za taifa katika Fungu A na alama husika kutoka katika Fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi, na kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi. Aidha, katika sehemu B, wanafunzi walitakiwa kujaza kabila au mkoa ambao kabila hilo hupatikana kwenye nafasi iliyoachwa wazi katika jedwali, kuchunguza picha kisha kujibu maswali na kusoma kwa makini kifungu cha habari kisha kuandika majibu katika sehemu zilizoachwa wazi.

Taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya upimaji wa somo la Uraia na Maadili imejikita katika kuangalia maswali yote sita yaliyotoka katika umahiri mbalimbali ulioainishwa katika muhtasari. Uchambuzi huu pia unabainisha idadi au asilimia ya wanafunzi walioweza au walioshindwa kuchagua jibu sahihi na sababu zilizowafanya wachague majibu hayo.

Viwango vya ufaulu kwa kila swali vimezingatia asilimia ya wanafunzi waliofaulu katika swali husika. Iwapo asilimia 0 – 33 ya wanafunzi waliweza kujibu swali hilo vizuri, kiwango cha ufaulu cha swali hilo kinahesabika kuwa ni hafifu. Kwa upande mwingine, kama wanafunzi walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 34 – 66, ufaulu kwa swali hilo unahesabika kuwa ni wa wastani na kiwango cha ufaulu kinahesabika kuwa ni kizuri iwapo watahiniwa walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 67 – 100. Aidha, chati za viwango vya ufaulu zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu wa wanafunzi, ambapo rangi ya kijani, njano na nyekundu zinawakilisha kiwango cha ufaulu kizuri, wastani na hafifu, mtawalia.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI


### 2.1 Sehemu A : Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) ambapo swali la 1 lilikuwa la kuchagua herufi ya jibu sahihi na lilikuwa na vipengele vitano ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 2. Jumla ya alama ilikuwa 10. Swali la 2 lilikuwa la kuoanisha maana ya maneno katika fungu A na maneno husika katika fungu B kwa kuandika jibu sahihi katika karatasi ya kujibia na ilikuwa na vipengele vinne ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 2. Hivyo, jumla ya alama ilikuwa 8. Swali la 3 lilikuwa na vipengele 4, kila kipengele kilikuwa na alama 2. Hivyo, jumla ya alama ilikuwa 8. Jumla ya alama katika sehemu hii ilikuwa 26.

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika sehemu hii

### 2.1.1 Swali la 1. Kuwa Mwadilifu.

Swali hili ndilo lililojibiwa vizuri zaidi ikilinganishwa na maswali mengine. Swali hili liliwataka wanafunzi kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika katika kisanduku. Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwadilifu*.Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa, wanafunzi 1, 200,450 (76.9%) walifaulu katika swali hili. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 1 umefanyika kama ifuatavyo:

(i) Yapi kati ya yafuatayo ni makundi maalumu?

A Wazee, watoto na walemavu

B Watoto, matajiri na walemavu

C Wafanyakazi, maalbino na wazee

D Watoto, akinababa na walemavu

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kusimamia Haki* na kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kutambua makundi maalumu yaliyopo katika jamii. Wanafunzi walioweza kubaini jibu sahihi, *A*, *Wazee, watoto na walemavu* walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya aina za makundi maalumu katika jamii. Aidha, wanafunzi hawa waliweza kutambua kundi maalum kutokana na umri wao, maumbile yao au viungo vyao vya mwili. Watu hawa wanaweza kuwa ni watu wenye umri mdogo (watoto) au mkubwa sana (wazee), walemavu wa viungo vya mwili, au wanawake. Walielewa pia kuwa makundi maalumu yanakumbana na changamoto mbalimbali katika jamii, baadhi ya changamoto hizo ni kama vile lugha za matusi, kudhalilishwa, ubakwaji na utumikishwaji wa kazi ngumu. Changamoto zingine ni kutokuwa na mazingira rafiki kwa walemavu, kashfa, kejeli, kuzomewa na mfumo dume uliopo katika jamii.

Wanafunzi waliochagua vipotoshi *B*, *Watoto, matajiri na walemavu* *C*, *Wafanyakazi, matajiri na wazee* *D*, *Watoto, akinababa na walemavu* hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya aina za makundi maalumu yaliyopo katika jamii. Kwa mfano, waliochagua kipotoshi *B, Watoto, matajiri na walemavu* hawakujua kuwa matajiri sio sehemu ya makundi maalumu, kwasababu ni watu wenye mali. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *C*, *Wafanyakazi, maalbino* na *wazee* hawakujua kuwa wafanyakazi ni kundi lililoajiriwa katika sekta za serikali au binafsi na wanalipwa ujira au mshahara. Aidha, kipotoshi *D*, *Watoto, akinababa na walemavu* kiliwavutia wanafunzi ambao hawakujua kuwa akina baba ni kundi la watu wazima wanaume ambalo sio kundi maalumu katika jamii. Wanafunzi walishindwa kubaini jibu sahihi kwa kutokuwa na uwezo wa kuchambua mambo yaani walishindwa kubaini kuwa kila kipotoshi kilikuwa na kundi moja au mawili ya watu wenye ulemavu.

(ii) Ni tendo gani linalooneshа uwajibikaji wa watoto katika familia?

A Kununua sare za shule

B Kusaidia kazi ndogondogo za nyumbani

C Kucheza mpira shuleni na nyumbani

D Kujisomea muda wote

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kutimiza Majukumu yake kwa Uwazi na Ukweli* na kililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kutambua matendo yanayoonesha uwajibikaji wa watoto katika familia. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi C, *Kusaidia kazi ndogondogo za nyumbani* walikuwa na uelewa juu ya maana ya wajibu wa watoto katika familia. Wanafunzi hawa walijua kuwa wajibu ni jambo linalomlazimu mtu kulitimiza ambalo hana hiari nalo katika kulifanya. Aidha uwajibikaji wa watoto katika familia ni pamoja na kusoma kwa bidii, kutii wazazi au walezi, kuwasaidia wengine na kuwapenda watu wengine.

Wanafunzi waliochagua vipotoshi *A*, *Kununua sare za shule, C*, *Kucheza mpira shuleni na nyumbani,* na *D*, *Kujisomea muda wote* hawakuwa na uelewa juu ya uwajibikaji wa watoto katika familia. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *A*, *Kununua sare za shule* walishindwa kutambua kuwa kununua sare za shule sio wajibu wa watoto bali ni wa wazazi au walezi. Watoto wana haki ya kununuliwa sare za shule. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *C*, *Kucheza mpira shuleni na nyumbani* walishindwa kuelewa kuwa kucheza mpira ni tendo linalooneshа kutendewa haki kwa watoto. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *D*, *Kujisomea muda wote,* walishindwa kubaini kuwa kujisomea muda wote kunamnyima mtoto fursa au nafasi ya kushiriki katika kusaidia kazi ndogondogo za nyumbani. Pia kunamnyima nafasi ya kuchangamana (kufanya mahusiano) na

watoto wengine katika jamii. Kujisomea kunatakiwa kuwa na muda maalumu uliopangiliwa vizuri.

(iii) Mahitaji matatu ya msingi ambayo yanapaswa kutolewa na wazazi kwa watoto wao ni pamoja na

A malazi, afya na ajira.

B kitanda, chakula na ulinzi.

C makazi, mkate na chakula.

D chakula, mavazi na malazi.

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kusimamia Haki.* Kililenga kupima umahiri wa wanafunzi katika kufahamu matendo yanayoonesha haki kwa watoto. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *D*, *chakula, mavazi na malazi*, walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya haki za watoto na namna ya kuzipata. Walijua kuwa haki maana yake ni hali ya kuwa mstahiki wa jambo. Walielewa kuwa kuna aina nyingi za haki za watoto, baadhi yake ni kama vile haki ya kuishi, haki ya kuendelezwa (kimwili, kiakili na kiroho), haki ya kulindwa (kuzuia vitendo viovu), haki ya kushiriki (kutoa mawazo na maamuzi) pamoja na haki ya kutobaguliwa (katika makundi mbalimbali).

Wanafunzi waliochagua vipotoshi *A*, *malazi, afya na ajira*, *B*, *kitanda, chakula na ulinzi* na *C*, *makazi, mkate na chakula* hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya matendo yanayoonesha haki kwa watoto. Walipaswa kuelewa kuwa *ajira,* kama inavyoonekana katika kipotoshi A ni kufanya kazi kwa ujira au malipo, *kitanda* katika kipotoshi B, ni kifaa kinachotumika kwa kulalia na *makazi* kwenye kipotoshi C ni mahali pa kuishi au makao. Vilevile walipaswa kuelewa kuwa *mkate* ni aina ya chakula kinachotengenezwa kwa kukandwa unga wa ngano, mtama, mahindi na kuokwa au kuchomwa. Baadhi ya mambo haya yaliyopo katika vipotoshi A, B na C kama vile afya, ajira, kitanda na mkate sio

ishara za haki za watoto zinazopaswa kutolewa na wazazi au walezi na wala sio mahitaji ya msingi kwa watoto katika familia.

(iv) Gabo alipokutana na bibi kizee, alimsalimia na kumsaidia kubeba mzigo wake. Tendo alilofanya Gabo ni kati ya matendo yanayoonesha nini?

A Kusaidia

B Uadilifu

C Wizi

D Woga

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahsusi wa *Kutimiza Majukumu yake kwa Uwazi na Ukweli* na kililenga kubaini matendo ya uadilifu yanayopaswa kufanywa na watoto katika jamii. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *B, Uadilifu* walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya uadilifu, walielewa kuwa uadilifu ni hali ya kuishi kwa kufuata maadili ya jamii. Aidha walijua kuwa uadilifu hujengwa na matendo ya uaminifu, ukweli, uwazi na kutenda haki.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliovutiwa na vipotoshi *A*, *Kusaidia C*, *Wizi* na *D*, *Woga* hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya matendo yanayoonesha uadilifu. Pia walishindwa kutofautisha kati ya kusaidia, wizi, woga na uadilifu. Walipaswa kujua kuwa *kusaidia* kutoka katika kipotoshi A, ni kufanya jambo la kumtoa mtu katika shida au kumwezesha kupata mahitaji yake au msaada. Waliochagua kipotoshi C, *Wizi* walishindwa kutambua kuwa wizi ni tendo lisilo la uaminifu. Matendo mengine yasiyo ya uaminifu ni kama vile kusema uongo, kuficha kitu kisicho chako na kushindwa kutimiza ahadi. Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi D, Woga hawakujua kuwa woga ni hali ya kuwa na hofu ya kufikwa na jambo la kutisha au la taabu. Hivyo, woga sio sehemu ya matendo

yanayoonesha uadilifu katika jamii. Uadilifu unasisitiza uwazi na ukweli.

(v) Pamela alitoa taarifa kwa mama yake kuwa alikuwa amevunja sahani. Tendo la kutoa taarifa alilolifanya Pamela linaonesha tabia gani?

A Kujipenda

B Kuwa na upendo

C Kuwa mkweli

D Kuwa na huruma

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kuaminika katika Jamii* na kililenga kubaini au kutambua matendo yanayoonesha uaminifu katika jamii. Wanafunzi waliobaini jibu sahihi *C*, *Kuwa mkweli* walikuwa na maarifa ya kutosha na walitambua kuwa ukweli maana yake ni uhalisia wa kinachosemwa au kutendwa. Ni uhalisia wa kitu bila kuongeza au kupunguza uhalisia huo. Matendo ya ukweli ni matokeo ya uaminifu ambayo yanahusisha mambo kama kutimiza ahadi, kutunza siri, kufichua uovu na kutunza mali uliyokabidhiwa.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua vipotoshi, *A, Kujipenda, B, Kuwa na upendo na D, Kuwa na huruma* walikosa maarifa ya kutosha kuhusu kutambua matendo ya uaminifu katika jamii. Aidha, walishindwa kubaini kuwa vipotoshi vyote hivi havina uhusiano wa moja kwa moja na matendo yanayoambatana na ukweli. Wanafunzi hawa walishindwa kujua kuwa kipotoshi A, *Kujipenda* kunamaanisha kukata shauri kufanya jambo kwa kuridhika mwenyewe, jambo ambalo sio mojawapo ya uaminfu. Waliochagua kipotoshi B, *Kuwa na upendo* walipaswa kujua kuwa upendo ni hali ya kuvutiwa na uzuri wa kitu. Hivyo, halihusiani na uaminifu. Wanafunzi waliovutiwa na kipotoshi *D, Kuwa na huruma*

walipaswa kujua kuwa huruma ni hali ya kuwa na moyo wa wema au rehema au upole. Aidha ni tendo linaloonesha kujali wengine lakini sio mojawapo ya matendo ya uaminifu. Mwisho uaminifu unaonekana pale mtu anapozingatia malengo yake ikiwemo ratiba binafsi.


### 2.1.2 Swali la 2 : Kuheshimu Jamii

Swali hili lilikuwa na vipengele (i) - (iv), liliwataka wanafunzi kuoanisha maelezo kuhusu alama za Taifa katika Fungu A na alama husika kutoka katika Fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

<table>
<tr><th colspan="2">Fungu A</th><th>Herufi</th><th>Fungu B</th></tr>
<tr><td>(i)</td><td>Alama inayowakilisha uhuru na nuru inayoangaza nchi yetu.</td><td>( )</td><td rowspan="4">A. Bendera ya Taifa<br>B. Fedha ya Taifa<br>C. Mwenge wa Uhuru<br>D. Mnyama wa Taifa<br>E. Nembo ya Taifa<br>F. Wimbo wa Taifa</td></tr>
<tr><td>(ii)</td><td>Alama yenye rangi nne ambazo ni kijani, bluu, nyeusi na manjano.</td><td>( )</td></tr>
<tr><td>(iii)</td><td>Alama inayoonesha picha ya mwanamke upande wa kushoto na kulia.</td><td>( )</td></tr>
<tr><td>(iv)</td><td>Alama inayoonesha uzalendo wa taifa letu.</td><td>( )</td></tr>
</table>

Swali hili lilikuwa na vipengele vinne kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu Jamii* na kwenye umahiri mahususi wa *Kuipenda Tanzania kwa Kuenzi Tunu za Nchi na Asili Yake*. Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi katika kutambua alama za taifa na maana zake**.** Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani**,** ambapo ni asilimia 54.8 tu ya wanafunzi 1,560,830 ndio waliweza

kupata kuanzia alama 4 hadi 8. Hivyo, asilimia 45.2 hawakufaulu, kwa kuwa walipata alama kuanzia 0 hadi 2. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2.




**Chati Na.2**: *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2*

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele:

Kipengele cha (i) kilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini alama ya taifa inayowakilisha uhuru na nuru inayoangaza nchi yetu. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *C*, *Mwenge wa Uhuru* walikuwa na uelewa juu ya alama za taifa na maelezo yake. Walielewa kuwa Mwenge wa Uhuru humaanisha uhuru na mwanga ambao humulika nchi na mipaka yake. Pia huleta tumaini palipo na kukata tamaa, upendo palipo na uadui na heshima palipo na chuki. Aidha, huwakumbusha Watanzania wajibu wao wa kuwa tayari kudumisha uhuru, umoja na amani.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi *A, Bendera ya Taifa* hawakuelewa kuwa Bendera ya Taifa ni kitambulisho cha kuonesha kuwa nchi ni huru na kwamba ina rangi nne ambazo ni rangi ya kijani, njano, nyeusi na rangi ya bluu. Waliochagua kipotoshi *B, Fedha ya Taifa,* hawakutambua kuwa Fedha ya Taifa haiwakilishi uhuru na nuru bali ni alama inayotambulisha fedha inayotumika nchini ambayo ni sarafu na noti. Baadhi ya wanafunzi waliochagua kipotoshi *D, Mnyama wa Taifa* hawakuwa na maarifa ya kutosha ya kuelewa kuwa Mnyama wa Taifa ni Twiga ambapo huwakumbusha Watanzania kuongeza uelewa wao kwa kuangalia maisha kutoka pande zote. Wanafunzi wengine walivutiwa na kipotoshi *E, Nembo ya Taifa* walishindwa kuelewa kuwa Nembo ya Taifa ni kielelezo cha umoja, uhuru na nguvu za taifa katika kujihami na kujilinda. Hivyo, Nembo ya Taifa haiwakilishi nuru inayoangaza nchi yetu. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *F, Wimbo wa Taifa* walishindwa kutambua kuwa *Wimbo wa Taifa* ni mojawapo ya alama za taifa ambayo huimbwa katika matukio muhimu ya kitaifa. Hivyo, sio alama inayowakilisha uhuru na nuru inayoangaza nchi yetu.

Kipengele cha (ii) kiliwataka wanafunzi kuoanisha maelezo yanayohusu alama ya taifa yenye rangi nne ambazo ni kijani, bluu, nyeusi na manjano. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi A, *Bendera ya Taifa* walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Bendera ya Taifa. Walijua kuwa hiyo ni alama ya utambulisho wa nchi iliyo huru. Pia, walifahamu kuwa Bendera ya Taifa ina rangi nne zenye maana tofauti. Yaani, rangi ya kijani humaanisha uoto wa mimea yetu, rangi ya njano huonesha madini yaliyo nchini mwetu, rangi nyeusi huwakilisha rangi ya Watanzania na rangi ya bluu humaanisha maji (bahari, maziwa na mito) iliyomo nchini mwetu.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi *B, Fedha ya Taifa,* hawakujua kuwa Fedha ya Taifa ni mojawapo ya alama za taifa na kwamba kuna aina kuu mbili za fedha nazo ni sarafu na noti. Hawakujua kuwa Fedha ya Taifa haiwakilishi taifa kwa njia ya rangi zake kama ilivyo kwa Bendera ya Taifa yenye rangi nne. Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi C*, Mwenge wa Uhuru* hawakuelewa kuwa Mwenge wa Uhuru, una umbo la koni na huwakilisha uhuru na nuru katika taifa letu. Mwenge huwakumbusha Watanzania kulinda uhuru, umoja na amani nchini mwetu.

Waliochagua kipotoshi D*, Mnyama wa Taifa* walipaswa kujua kuwa mnyama wa taifa ni Twiga. Alama hii huwakumbusha Watanzania kutumia nguvu zao na wawe na uwezo wa kubadilika ili kuendana na mazingira halisi kimwili, kiakili na kiroho kama alivyo Twiga. Wanafunzi waliochagua kipotoshi E*, Nembo ya Taifa* hawakujua kuwa Nembo ya Taifa ni kielelezo cha umoja, uhuru na nguvu za taifa. Wakati mwingine Nembo hii hutumika kama mhuri wa taifa katika ofisi za serikali. Waliovutiwa na kipotoshi F, *Wimbo wa Taifa* walipaswa kujua kuwawimbo huu huimbwa wakati wa matukio maalumu. Aidha wimbo wa taifa umetaja baadhi ya tunu za Taifa kama vile; amani na umoja.

Kipengele cha (iii) kiliwataka wanafunzi kutambua alama inayoonesha picha ya mwanamke na mwanaume upande wa kushoto na kulia. Wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi *F, Nembo ya Taifa* walikuwa na uelewa sahihi wa alama za taifa. Walijua kuwa alama ya taifa inayoonesha mwanaume na mwanamke kushoto na kulia ni Nembo ya Taifa. Walijua kuwa Nembo ya Taifa ni kielelezo cha umoja, uhuru na nguvu za taifa katika kujihami na kujilinda. Nembo ya Taifa ina Bendera ya Taifa, shoka, jembe, mwenge, pembe za ndovu, mkuki, mawimbi ya

bahari, Mlima Kilimanjaro, kaulimbiu ya “uhuru na umoja”, rangi ya manjano na rangi nyekundu.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi *A, Bendera ya Taifa,* hawakuwa na uelewa sahihi wa alama za taifa. Hawakutambua kuwa Bendera ya Taifa hupepea katika maeneo maalumu kama vile ofisi za serikali na hupandishwa asubuhi saa 12 na kushushwa jioni saa 12. Inapopandishwa au kushushwa watu husimama wima kama ishara ya kuliheshimu taifa. Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi *B, Fedha ya Taifa*, hawakuwa na uelewa unaohusiana na alama za taifa, walipaswa kujua kuwa Fedha ya Taifa hutumia neno shilingi na iko katika mfumo wa sarafu na noti. Pia ilianza kutumika mwaka 1966. Kipotoshi *C, Mwenge wa Uhuru* kilichaguliwa na wanafunzi walioshindwa kuelewa kuwa Mwenge wa Uhuru huwakumbusha watanzania wajibu wao wa kuwa na wivu wa kulinda uhuru, umoja na amani katika nchi yao. Humulika mipaka, huleta tumaini, upendo na heshima kwa Watanzania wote.

Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi *D, Mnyama wa Taifa* hawakuelewa kuwa Mnyama wa Taifa ni Twiga na hulindwa kisheria. Maelezo ya mnyama twiga ni kuwa Watanzania waone maisha kutoka katika kila pande ili waweze kufanikiwa. Yaani hata kama wanaenda mbele wasisite kukumbuka nyuma, kujua ni wapi wametoka na nini wanatakiwa kufanya ili kufanikiwa kwa kipindi hicho. Vilevile, wanafunzi wengine waliochagua *kipotoshi F*, *Wimbo wa Taifa* hawakufahamu kuwa Wimbo wa Taifa jina lake ni “Mungu Ibariki Afrika”. Jina linatokana na maneno yake ya kwanza. Wimbo huu ulitungwa na Enoch Sentonga na ulinza kutumika mnamo mwaka 1961. Matumizi makubwa ya wimbo huu ni kuonesha umoja na undugu wa Waafrika na pia ni sala ya kuliombea Taifa la Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Kipengele (iv) kiliwataka wanafunzi kubaini alama inayoonesha uzalendo kwa taifa letu. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *F, Wimbo wa Taifa* walikuwa na uelewa sahihi juu ya alama ya taifa inayoonesha uzalendo wa taifa letu. Walitambua kuwa alama za taifa ni vitambulishovya taifa kati ya mataifa mengine. Pia vinawakilisha umoja na ufahari wa nchi. Walijua kuwa Wimbo wa Taifa ni alama ya taifa ambayo huimbwa wakati wa matukio muhimu ya kitaifa mfano, Rais, Makamu wa Rais au Waziri Mkuu anapotembelea nchi za nje. Aidha, rais wa nchi nyingine anapotembelea nchi yetu, kabla au baada ya kumaliza hotuba, inapotokea kifo cha Rais na wakati timu ya taifa inapocheza na timu ya taifa lingine. Wimbo wa Taifa hutoa ujumbe mbalimbali kama vile kuliombea mema bara la Afrika na viongozi wake, Mungu kutupa Baraka na kudumisha uhuru na umoja wa Watanzania.

Kwa upande mwingine**,** Wanafunzi waliochagua Kipotoshi *A, Bendera ya Taifa* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maana na umuhimu wa Bendera ya Taifa. Walitakiwa kujua kuwa Bendera ya Taifa ni kitambaa chenye rangi nne zenye maana tofauti. Bendera ya Taifa ni utambulisho kuwa nchi ni huru. Waliochagua kipotoshi B, *Fedha ya Taifa* hawakuwa na uelewa wa kutosha kwamba Wimbo wa Taifa huonesha uzalendo. Walitakiwa kujua kuwa Fedha ya Taifa ni miongoni mwa alama za taifa ambapo inatumia neno shilingi na imegawanyika katika sarafu na noti. Fedha ya Taifa ina noti ya shilingi 1000, 2000, 5000 na 10,000. Aidha, ina sarafu ya shilingi 50,100, 200 na 500.


Wanafunzi waliovutiwa na kipotoshi C, *Mwenge wa Uhuru* hawa kujua kuwa Mwenge wa Uhuru huwakilisha uhuru na nuru inayoangaza nchi yetu pamoja na kumulika mipaka, kuleta tumaini,

upendo heshima kwa taifa lote. Huwakumbusha Watanzania wote kuwa tayari kulinda uhuru, umoja na amani.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Mnyama waTaifa,* walitakiwa kujua kuwa Mnyama wa Taifa ni Twiga. Twiga hutoa ujumbe kwa Watanzania wote kutumia nguvu zao ili kufanikiwa katika maisha. Huwakumbusha kuyaona maisha kutoka katika kila upande ili waweze kufanikiwa. Aidha wanafunzi wengine walivutiwa na kipotoshi E, *Nembo ya Taifa*. Wanafunzi hawa hawakujua kuwa Nembo ya Taifa ni kielelezo cha umoja, uhuru na nguvu ya taifa katika kujihami na kujilinda. Nembo ya Taifa ina sehemu kuu nne: sehemu ya dhahabu (ina Mwenge wa Uhuru), sehemu yenye Bendera ya Taifa (rangi nne, kijani, njano, nyeusi na buluu), sehemu yenye rangi nyekundu (inamaanisha ardhi), sehemu ya milia ya buluu na nyeupe (mawimbi ya bahari na maziwa).

### 2.1.3 Swali la 3: Kuithamini Jamii

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu *Kuithamini Jamii.* Liliwataka wanafunzi kuchagua jibu sahihi kutoka katika mabano na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi. Swali lilikuwa na vipengele vinne kutoka katika umahiri mahususi mbalimbali. Kila kipengele cha swali hili kilikuwa na alama 2. Ufaulu wa wanafunzi katika Swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 1,041,582 (66.8%) waliweza kupata alama 4 hadi 8. Wanafunzi 519,248 (33.2%) hawakufanya vizuri kwa sababu walipata alama kuanzia 0 hadi 2. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika vipengele vinne vya maswali ni kama ifuatavyo:

(i) Njia mojawapo ya kuhifadhi mazingira yetu ni____________________ (kukata miti, kuchoma misitu, kupanda miti)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kutunza Mazingira na Vilivyomo.* Swali lililenga kupima ufahamu wa mwanafunzi juu ya dhana na matendo yanayoonesha njia za kuhifadhi mazingira yetu. Wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi *kupanda miti* walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya kuhifadhi mazingira. Wanafunzi hawa walielewa kuwa kupanda miti ni njia mojawapo inayotumika kuhifadhi ardhi. Walielewa kuwa hifadhi ya mazingira ni juhudi zinazofanywa na binadamu ili kuhakikisha sehemu anapoishi

haiharibiwi. Vilevile walielewa njia nyingine za kuhifadhi mazingira kuwa ni kutokata miti ovyo, kutochoma misitu, kutofuga mifugo mingi katika eneo dogo na kupanda mazao yanayoongeza rutuba kwenye ardhi. Aidha walielewa kuwa ukataji wa miti ovyo unaathari nyingi ikiwemo ukosefu wa mvua na kuongezeka kwa joto.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa kubaini jibu sahihi walivutiwa na vipotoshi *kukata miti na kuchoma misitu*. Wanafunzi hawa hawakuelewa kuwa dhana zote mbili zinaharibu mazingira. Njia nyingine zinazoharibu mazingira yetu ni kama vile kilimo kisichofaa, uchimbaji wa madini, uvunaji wa miti, umaskini, ongezeko la haraka la watu, upangaji usiofaa wa makazi na matumizi mabaya ya kemikali za viwandani. Aidha uharibifu wa mazingira unaweza kuzuiwa kwa kufanya yafuatayo: kutoa elimu ya mazingira kwa wananchi, upandaji wa miti, upunguzaji wa mifugo, matumizi ya nishati mbadala, kilimo rafiki na kuondoa umaskini.

(ii) Amani anatapika. Yawezekana anasumbuliwa na

______________________________

(maumivu ya mguu, ugonjwa wa malaria, ugonjwa wa ngozi)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kujijali na Kuwajali Wengine.* Lengo la swali lilikuwa kupima uwezo wa mwanafunzi katika kubaini aina mbalimbali za magonjwa na dalili zake. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *ugonjwa wa malaria waliweza* kutofautisha dalili mbalimbali za magonjwa. Wanafunzi hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu ugonjwa wa malaria. Waliweza kujua kuwa ugonjwa wa malaria unaambukizwa na mbu aina ya anopheles ambaye husababisha homa kali. Aidha, walitambua kuwa ugonjwa huu una dalili kama vile kuhisi baridi isiyo ya kawaida na kutetemeka, maumivu ya kichwa na udhaifu wa mwili, joto jingi mwilini, kutokwa na

jasho joto, kutapika na maumivu ya misuli au viungo. Aidha walikuwa na ufahamu juu ya madhara ya malaria kwa afya kama vile kuvimba kwa mishipa ya damu ya kwenye ubongo, kujaa maji kwenye mapafu, kushindwa kufanya kazi kwa figo, maini au bandama, upungufu wa damu na upungufu wa sukari mwilini.

Kwa upande mwingine, wanafunzi ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha walivutiwa na kipotoshi *maumivu ya mguu.* Wanafunzi hawa hawakujua kuwa maumivu ya miguu yanaweza kuwa maumivu ya kisigino, maumivu ya misuli ya miguu, kukaza kwa kano za miguu na miguu kuhisi ganzi. Aidha, miguu ni eneo gumu na ya juu inayojumuisha kano, misuli, viungo na mishipa ambapo miundo yote ina jukumu la kufanya kazi vyema wakati wa kusimama na kutembea. Maumivu ya miguu yanaweza kusababishwa na misuli kujikunja au kuvunjika. Waliochagua kipotoshi *ugonjwa wa ngozi* walishindwa kutambua kuwa unaweza kusababishwa na aina ya vyakula, vinywaji, jua, bakteria, aleji au ugonjwa wa kisukari. Ugonjwa wa ngozi unaweza kuonekana kwenye uso, kichwa, shingo, mabega na kwenye ngozi. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kuwa ugonjwa wa ngozi unaweza kufanya ngozi kuwa na rangi nyekundu au nyeupe, ngozi kuwa ngumu, mwasho, vidonda vya wazi, ngozi kuwa kavu na kupasuka, kupoteza rangi ya ngozi, vipele, mapunye na chunusi.

(iii) Kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla ya kula ni kitendo cha________________________________
(uaminifu, kujijali, heshima)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kujijali na Kuwajali Wengine* na kililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kubaini matendo ya kujijali. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *kujijali* walikuwa na uelewa wa kutosha wa maana ya kujijali. Baadhi ya matendo ya


kujijali ni kama vile kujiheshimu, kujikinga na mambo yanayoweza kukuletea madhara, kufanya mazoezi ya viungo kila siku, mtoto kushusha chandarua kabla ya kulala, kupiga mswaki, kupiga pasi nguo na kuoga kila siku.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua vipotoshi *uaminifu na heshima. H*awakuweza kutofautisha kati ya dhana ya uaminifu na heshima. Wanafunzi waliochagua *uaminifu* hawakuelewa kuwa uaminifu ni tabia ya mtu kuweza kuaminika na hujengwa kwa kutenda matendo kama vile kuwa mkweli, kutangaza kitu ulichookota, kurudisha pesa kamilifu iliyobaki baada ya kununua ulichoagizwa, kutimiza ahadi, kutoa ushauri unaofaa na kutoa taarifa za uhalifu. Aidha, matendo ya kukosa uaminifu ni kama vile kushiriki matendo ya wizi, kutotoa taarifa sahihi, kutofanya maamuzi sahihi na thabiti na kuwa na mtazamo hasi dhidi ya jambo zuri. Waliochagua *heshima* hawakujua kuwa heshima ni thamani ya utu. Heshima ni kitu anachopewa mtu kama alama ya kuthaminiwa. Heshima inatarajiwa kutoka kwa watu wenye sifa na maadili bora. Mara nyingi heshima huendana na usikivu na utiifu. Hujengwa kwa kufanya vitu vinavyogusa maisha ya watu, kuwakubali watu na kuomba msamaha unapokosea. Aidha, mambo yanaweza kumfanya mtu kukosa heshima ni pamoja na muonekano usioridhisha unaojumuisha usafi wa mavazi na mwili, kauli zisizo na busara, utendaji wa kazi, kutotimiza ahadi, sifa zisizo na maana na kutokuwa mwaminifu.

(iv) Ili familia iweze kujipatia mahitaji yake muhimu inatakiwa kufanya nini? ____________________________

(Kukata miti, Kufanya kazi kwa bidii, Kuhifadhi fedha benki)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kujijali na Kuwajali Wengine*, na kililenga kupima uelewa wa wanafunzi juu ya umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii. Wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi *kufanya kazi kwa bidii* walionesha uelewa wa maana ya kufanya kazi kwa bidii (kuwa ni kuonesha juhudi katika utendaji wa kazi ilikupata mahitaji muhimu katika maisha). Pia waliweza kubaini faida za kufanya kazi kwa bidii kama vile kufikia malengo uliojiwekea, kuheshimika, kupata mahitaji yako ya msingi, kutambulika, kupata matokeo makubwa, kuboresha afya na kuondoa lawama na manungu'niko. Waliweza kubaini kuwa kinyume cha kuwa na bidii ni kuwa mvivu, ikimaanisha kuwa mzito kutekeleza wajibu na mambo ambayo yanaweza kukuletea maendeleo. Uvivu unaambatana na hali ya kupenda usingizi au kupumzika wakati wengine wakifanya kazi. Kielelezo Na.3.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika majibu sahihi katika swali hili.


3. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Njia mojawapo ya kuhifadhi mazingira yetu ni Kupanda miti.
(kukata miti, kuchoma misitu, kupanda miti)

(ii) Amani anatapika. Yawezekana anasumbuliwa na ugonjwa wa malaria.
(maumivu ya mguu, ugonjwa wa malaria, ugonjwa wa ngozi)

(iii) Kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla ya kula ni kitendo cha Kujijali.
(uaminifu, kujijali, heshima)

(iv) Ili familia iweze kujipatia mahitaji yake muhimu inatakiwa kufanya nini? Kufanya kazi kwa bidii.
(kukata miti, kufanya kazi kwa bidii, kuhifadhi fedha benki)

**Kielelezo Na. 3.1:** *Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 3*

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi *kukata miti*, hawakujua kuwa kukata miti ni njia mojawapo ya njia inayoharibu mazingira. Uharibifu wa mazingira huambatana na athari nyingi kwa maisha ya mwanadamu na mazingira kwa ujumla, kwa mfano, kuwa chanzo cha mabadiliko ya hali ya hewa, kuongezeka kwa kiwango cha hewa ya ukaa, nchi kugeuzwa jangwa, kutokea kwa mmomonyoko wa udongo, kupotea kwa viumbe anuwai vilivyopo katika mazingira na kukosekana kwa mvua ya uhakika. Aidha, wanafunzi hawa walipaswa kujua umuhimu wa kuhifadhi miti/misitu. Faida hizo ni kama vile kuzuia athari ya uchafu, uhifadhi wa rutuba ya udongo, kudumisha kiwango cha maji kinachohitajika chini ya ardhi, kufanya hali ya hewa kuwa nzuri zaidi kwa wanadamu, wanyama, ndege na wadudu. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *kuhifadhi fedha benki* hawakuelewa kuwa hiki ni kitendo cha kutunza pesa kwa ajili ya malengo ya baadaye ambayo mtu anatamani kuyafanikisha. Ni njia mojawapo salama na ya uhakika ya kuhifadhi fedha. Waliochagua kipotoshi hiki walikwenda nje na mahitaji ya swali ambayo ni umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii. Kielelezo Na 3.2 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 3

3. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Njia mojawapo ya kuhifadhi mazingira yetu ni Jarorani Kupanda.
(kukata miti, kuchoma misitu, kupanda miti)

(ii) Amani anatapika. Yawezekana anasumbuliwa na Kawiku maumivu yangu.
(maumivu ya mguu, ugonjwa wa malaria, ugonjwa wa ngozi)

(iii) Kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla ya kula ni kitendo cha uaminifu.
(uaminifu, kujijali, heshima)

(iv) Ili familia iweze kujipatia mahitaji yake muhimu inatakiwa kufanya nini? Kwadi Kabidii.
(kukata miti, kufanya kazi kwa bidii, kuhifadhi fedha benki)

**Kielelezo Na.3.2**: *Sampuli ya majibu yasiyosahihi ya mwanafunzi katika swali la 3*

## 2.2 Sehemu B : Maswali ya Majibu Mafupi


Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) swali la 4, 5, na 6. Swali la 4 liliwataka wanafunzi kuandika kabila au mkoa ambao kabila hilo hupatikana, wakati kipengele (i) kilitolewa kama mfano. Jumla ya alama katika swali hili ilikuwa alama 8. Swali la 5 lilikuwa la kuchunguza picha kisha kujibu maswali yanayofuata. Lilikuwa na alama 8. Swali la 6 lilikuwa la kusoma kifungu cha habari kisha kujibu vipengele (i) – (iv) kwa kuandika majibu katika sehemu zilizoachwa wazi. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 8.

### 2.2.1 Swali la 4: Kudumisha Amani

Swali hili lilikuwa na vipengele (ii) – (v), liliwataka wanafunzi kujaza kabila au mkoa ambao kabila hilo hupatikana kwenye nafasi zilizoachwa wazi katika jedwali. Namba (1) ilitolewa kama **mfano**.

| Na. | Kabila | Mkoa |
|---|---|---|
| (i) | ***Wapogoro*** | ***Morogoro*** |
| (ii) | Wagogo | |
| (iii) | | Mwanza |
| (iv) | | Tabora |
| (v) | Wahaya | |

Swali lilikuwa na vipengele vinne; (ii) (iii), (iv) na (v), vilivyotoka katika umahiri mkuu wa *Kudumisha Amani,* kwenye umahiri mahususi *Kuheshimu Tofauti za Kiutamaduni na Mitazamo Miongoni mwa Watu wa Jamii Tofauti*. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kutambua makabila au mikoa ambako makabila hayo hupatikana. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani, wanafunzi 264,482 (16.89%) walipata alama kuanzia 4 hadi 8, na wanafunzi 1,296,348 (83.11%) hawakufaulu, kwa kuwa walipata alama kuanzia 0 hadi 2. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4*

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele

Kipengele (ii) kiliwataka wanafunzi kubaini mkoa ambao kabila la Wagogo linapatikana nchini Tanzania. Wanafunzi waliobainisha kuwa ni Mkoa wa Dodoma, walikuwa na maarifa ya kutosha kutambua kabila na mkoa ambao kabila hilo hupatikana. Aidha, walitambua makabila mengine yanayopatikana mkoani Dodoma kuwa ni Wakaguru katika wilaya ya Kongwa na Mpwapwa, Warangi na Wasandawe katika wilaya ya Kondoa. Makabila mengine yanayopatikana mkoani Dodoma ni Wanguu, Wabununge, Wafyomi, Wahadzabe na Wabarbaig. Vilevile walitambua kuwa makabila haya hujishughulisha na shughuli za kiuchumi kama vile kilimo cha mazao yanayovumilia ukame kama mtama na mhogo. Mazao mengine ni kama vile mahindi, karanga, alizeti na zabibu. Pia hushiriki katika shughuli za ufugaji wa ng’ombe, kondoo, mbuzi, nguruwe na kuku. Shughuli zao nyingine ni uwindaji na urinaji wa asali.

Aidha, wanafunzi wengine walishindwa kubaini kuwa Wagogo wanapatikana mkoani Dodoma. Wanafunzi hawa waliandika mikoa mingine ambayo haikuwa asili ya kabila la Wagogo. Wanafunzi hao walikosa maarifa ya kubaini mkoa sahihi ambao kabila hilo hupatikana. Baadhi ya wanafunzi waliandika Dar es Salaam, Mwanza, Rukwa na Tabora. Wanafunzi hawa hawakuelewa kuwa wenyeji wa Mkoa wa Dar es Salaam ni Wazaramo, Mkoa wa Mwanza ni Wasukuma, mkoa wa Rukwa ni Wafipa na Mkoa wa Tabora ni Wanyamwezi. Wanafunzi hawa vilevile, walipaswa kujua kuwa shughuli za asili za kiuchumi zinaweza kusaidia kutambua mkoa na kabila husika. Kwa mfano, Wapare kutoka Mkoa wa Kilimanjaro wanajihusisha na ufinyanzi wa vyungu, Wamakonde kutoka Mtwara hushiriki katika shughuli za uchongaji wa vinyago na Wakerewe kutoka Mkoa wa Mwanza huhusika na uvuvi wa samaki.

Kipengele (iii) kiliwataka wanafunzi kujaza kabila linalopatikana Mkoani Mwanza. Wanafunzi waliobaini *Wasukuma* walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kabila linalopatikana mkoani humo. Walielewa kuwa Wasukuma wamesambaa katika wilaya za Sengerema, Magu, Kwimba, Misungwi na Ilemela. Aidha, Wakerewe na Wakara wanapatikana sana katika Wilaya ya Ukerewe, mkoani Mwanza. Mbali na Wasukuma na Wakerewe, makabila mengine mkoani humo ni pamoja na Wazinza, Wasumbwa, na Walongo. Aidha walijua kuwa shughuli kuu za kiuchumi zinazo fanyika mkoani Mwanza ni kilimo, ufugaji na uvuvi wa samaki kutoka Ziwa Viktoria.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walikosa uelewa wa kabila linalopatikana Mkoani Mwanza kuwa ni Wasukuma. Wanafunzi hawa waliandika makabila kama vile Wagogo, Wahaya, Warangi na Wazanaki. Walishindwa kutambua kuwa Wagogo na Warangi wanapatikana Mkoani Dodoma, Wahaya wanapatikana Mkoani Kagera na Wazanaki wanapatika Mkoani Mara.

Kipengele (iv) kiliwataka watahiniwa kuandika kabila linalopatikana Mkoa wa Tabora. Wanafunzi waliokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu kabila linalopatikana kutoka Mkoa wa Tabora, waliweza kubaini kuwa ni W*anyamwezi.* Aidha waliweza kujua kuwa, sio Wanyamwezi pekee wanaoishi mkoani humo bali kuna makabila mengine kama vile Wasukuma, Waha, Wanyakyusa na Wachaga. Pia walijua kuwa shughuli kuu za kiuchumi za makabila mengi yanayopatikana katika Mkoa waTabora ni kilimo na ufugaji. Mazao yanayolimwa ni kama vile tumbaku, mpunga, viazi vitamu, mahindi, mtama, pamba, alizeti na karanga. Pia, wanajishughulisha na ufugaji wa ng’ombe, mbuzi, kondoo na ufugaji wa kuku.

Kwa upande mwingine, Wanafunzi wengine kwa kukosa ufahamu waliandika makabila yasio sahihi kwa Mkoa wa Tabora. Baadhi yao waliandika kabila la Wahehe, Wapare, Wakerewe na Wamakonde. Walishindwa kujua kuwa, Wahehe ni kabila linalopatikana Mkoani Iringa, Wapare wanapatikana Mkoa wa Kilimanjaro, Wakerewe wanapatikana Mkoa wa Mwanza na Wamakonde wanapatikana Mkoa wa Mtwara.

Kipengele (v) kiliwataka wanafunzi kubainisha mkoa wanakopatikana Wahaya. Wanafunzi waliokuwa na ufahamu wa kutosha waliandika mkoa wa Kagera. Wanafunzi hawa waliweza kubaini kuwa Wahaya wanapatikana Mkoa wa *Kagera* pia*,* walielewa kuwa makabila mengine yanayo patikana Mkoa wa Kagera ni Wanyambo wanaopatikana wilaya ya Karagwe na Kyerwa, Wasubi Wilaya ya Biharamulo na Wahangaza kutoka wilaya ya Ngara. Pia kuna makabila mengine kama vile Waha, Wazinza na Warongo. Chakula kikuu cha makabila ya Kagera ni ndizi na maharage. Shughuli zao kuu za kiuchumi ni kilimo cha migomba, kahawa miwa, mahindi, mihogo na mboga. Pia wanajishughulisha na kazi za uvuvi kutoka Ziwa Viktoria. Wapo wachache wanafuga mifugo kama ng’ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku. Kielelezo Na.4.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi.

4. Jibu vipengele (ii) - (v) kwa kujaza Kabila au Mkoa ambao kabila hilo hupatikana kwenye nafasi zilizoachwa wazi katika Jedwali. Namba (i) imetolewa **kama mfano.**

| Na. | Kabila | Mkoa |
|---|---|---|
| (i) | ***Wapogoro*** | ***Morogoro*** |
| (ii) | Wagogo | Dodoma |
| (ii) | Wasukuma | Mwanza |
| (iv) | Wanyamwezi | Tabora |
| (v) | Wahaya | Kagera |

**Kielelezo 4.1:** *Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4*

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioandika mikoa mingine kama vile, Mbeya, Iringa, Kigoma na Singida kama mikoa ambako Wahaya wanapatikana hawakujua kuwa kabila linalopatikana katika Mkoa wa Mbeya ni Wanyakyusa, Mkoa wa Iringa Wahehe na Wabena, Kigoma Waha na Singida, Wanyiramba. Wanafunzi hawa walitakiwa kujua kuwa ni muhimu kufahamu vizuri makabila yanayopatikana Tanzania ikiwa ni pamoja na makazi yao, ngoma zao za asili, vyakula, lugha and shughuli kuu za kiuchumi. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu yasio sahihi ya mwanafunzi.

4. Jibu vipengele (ii) – (v) kwa kujaza Kabila au Mkoa ambao kabila hilo hupatikana kwenye nafasi zilizoachwa wazi katika Jedwali. Namba (i) imetolewa **kama mfano.**

| Na. | Kabila | Mkoa |
|---|---|---|
| (i) | ***Wapogoro*** | ***Morogoro*** |
| (ii) | Wagogo | Tarime |
| (ii) | Watugera | Mwanza |
| (iv) | Wamasai | Tabora |
| (v) | Wahaya | Dar as alamu |

**Kielelezo 4.2** *Sampuli ya majibu yasiyosahihi ya mwanafunzi katika swali la 4*

### 2.2.2 Swali la 5 Kuwa Mstahimilivu

Swali hili lilikuwa la kuchunguza picha kisha kujibu maswali yanayofuata**.**



**Maswali**

(a) Wanafunzi kwenye picha hii wanafanya nini?

______________________________________

(b) Unafikiri watoto hawa wapo katika mazingira yapi?

___________________________________________


(c) Ni faida ipi unayoweza kuipata unaposhiriki katika tendo lilioneshwa katika picha?

___________________________________________

(d) Taja jina la samani iliyopo katika picha ambayo hutumiwa kuhifadhia vitabu.

_________________________________________

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mstahimilivu* na umahiri mahususi wa *Kujifunza kwa Kuchanganua Mambo Kiyakinifu.* Swali lililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu manufaa ya kujifunza kwa njia ya makundi. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne na kila kipengele kilikuwa na alama 2. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo wanafunzi 1,050,718 (67.3%) walipata alama kuanzia 4 hadi 8, na wanafunzi 510,112 (32.7%) walipata alama kuanzia 0 hadi 2 kama inavyooneshwa kwenye Chati.Na.5




**Chati Na.5:** *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 5*

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele:

(a) Wanafunzi kwenye picha hii wanafanya nini? ______________________

Kipengele hiki kililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu aina ya tendo linalofanyika katika picha. Wanafunzi waliojibu *wanajifunza/wanajisomea/wanajadiliana kwa makundi,* walikuwa na ufahamu wa kutosha juu ya tendo linalofanyika katika picha. Walijua kuwa majadiliano kwa makundi ni aina ya mazungumzo yanayohusisha watu wanaobadilishana mawazo. Wanaojadiliana wanaunganishwa na jambo moja la msingi, kutokana na jambo hilo kila mmoja katika kundi huwasilisha mawazo au maoni yake. Aidha walijua kuwa lengo la majadiliano kwa makundi ni kutatua au kupata suluhu juu ya jambo husika. Vilevile ni kupata mawazo mapya ya kutatua tatizo lililo mbele yao.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi ambao walipata alama 0 katika kipengele hiki, walishindwa kubaini matakwa ya swali. Hivyo walitoa aina mbalimbali za majibu ambayo siyo sahihi kama vile, *wanaandika, wanajisomea, wanawasiliana na wanalinganisha* Wanafunzi walioandika *wanaandika w*alishindwa kubaini tendo lililokuwa linaendelea katika picha. Kuandika ni kufanya/kuumba au kuchora kwa kutumia herufi kuwakilisha sauti. Pia, wengine walikosa stadi za KKK hivyo kuandika majibu yasiyoeleweka kama *ukimupi, unjggopea, kimik na wan aka.*

(b) Unafikiri watoto hawa wapo katika mazingira yapi?

Kipengele hiki kililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu mazingira au sehemu sahihi ambapo majadiliano kwa njia ya makundi yanaweza kufanyika. Wanafunzi wenye ufahamu wa kutosha waliweza kubaini kuwa sehemu/mazingira sahihi ni *shuleni* au *darasani.* Mazingira haya yanaonesha ni rasmi kwa kujifunza. Wanafunzi kuvaa sare, vitabu/madaftari, kalamu, viti na meza vinadhihirisha kuwa ni mazingira ya shuleni au darasani.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliopata alama 0 walishindwa kubaini matakwa ya swali kwa kuandika aina mbalimbali za majibu ambayo sio sahihi. Majibu yao yalikuwa kama vile *mazingira ya kujisomea, ya kujadiliana, mazingira ya kufundishana, kucheza pamoja, wapo katika mazingira safi na wapo mazingira ya usiku.* Wanafunzi walioandika *mazingira ya kujisomea* walishindwa kujua kuwa kujisomea kunahusisha nafsi moja na utulivu hivyo kuwa tofauti na kinachofanyika katika picha. Wanafunzi waliotaja *kucheza pamoja,* hawakujua kuwa kucheza kunahusisha kitu cha kuchezea kinachoweza kuwa kamba, mpira au kopo au uwanja, mazingira yaliyo tofauti na kinachofanyika katika picha. Vilevile, wanafunzi

walioandika *wapo katika mazingira ya usiku* walishindwa kutafsiri sawasawa matendo yanayofanyika na kushindwa kubaini muda halisi wa kitendo kinachofanyika kwenye picha waliyopewa. Mwisho, wanafunzi wengine walinakili tu maswali yaliyoulizwa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika *unafikiri watoto hawa wapo katika mazingira yapi*, badala ya kujibu swali aliloulizwa.

(c) Ni faida ipi unayoweza kuipata unaposhiriki katika tendo lilioneshwa katika picha?


Kipengele hiki kililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu faida inayoweza kupatikana kutokana na kushiriki katika tendo lililooneshwa katika picha ambalo ni *kujifunza kwa makundi au kujadiliana kivikundi au kujisomea kwa makundi au kujifunza kwa makundi*. Wanafunzi wenye maarifa ya kutosha waliweza kubaini faida ya majadiliano kwa makundi ambayo ni kubadilishana maoni baina ya washiriki kwenye umahiri husika. Wanafunzi hawa walijua faida nyingi zinazotokana na majadiliano kwa makundi. Baadhi ya faida hizo ni kama vile *Kubadilishana uzoefu, kukuza vipaji, kukuza ushirikiano, kufanya kazi kwa pamoja, kujenga hali ya kujiamini, kukuza upendo, kukuza mshikamano, kuaminiana, kupata mawazo mengi juu ya umahiri husika, husaidia kutambua makosa yako na udhaifu ulionao, kupata mrejesho juu ya utendaji na kujenga mawasiliano thabiti.*

Kwa upande mwingine, badhi ya wanafunzi waliopata alama 0 katika kipengele hiki walishindwa kubaini matakwa ya swali na hivyo kushindwa kuandika maneno yanayoeleweka. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika *kukaa pamoja, kusoma nikiwa shuleni,*

*kusoma kwa bidii, kukaa wote wa shule*, *elimu kwa bidii*. Wanafunzi wengine waliandika *kuwa na heshima*, *unaweza kujifunza kusoma na kuandika*, *kuwa na kipaji* na *kujua kusoma*.

(d) Taja jina la samani iliyopo katika picha ambayo hutumiwa kuhifadhia vitabu ___________________________

Kipengele hiki kilipima ufahamu wa wanafunzi katika kutambua aina ya samani iliyopo katika picha ambayo hutumika katika kuhifadhi vitabu. Wanafunzi wenye maarifa ya kutosha waliweza kubaini samani hiyo kuwa ni *Kabati.* Walijua kuwa Kabati ni aina ya sanduku kubwa la wima linalotengenezwa kwa mbao au chuma au glasi au bati kwa ajili ya kuhifadhia nguo, vyombo, vyakula, vitabu au nyaraka mbalimbali. Kwa kawaida, kabati huwekwa ofisini*,* chumba cha kusomea, maktaba au darasani au sebuleni, au jikoni*.* Wanafunzi hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kuwa na kabati. Baadhi ya faida hizo ni kama vile kusaidia kutunza vitabu na machapisho mengineyo, kuwekea na kutunzia nguo, kuwekea vyombo na runinga. Kielelezo Na.5.1 kinaonesha majibu sahihi ya mwanafunzi.



**Maswali**

(a) Wanafunzi kwenye hii picha wanafanya nini?

Wanafunzi wana jadili kwa vikundi.

(b) Unafikiri watoto hawa wapo katika mazingira yapi?

Watoto hawa wapo katika mazingira ya shuleni.

(c) Ni faida ipi unayoweza kuipata unaposhiriki katika tendo lilioneshwa katika picha?

faida unayoweza kuipata ni kuelimika endapo utatia bidii.


(d) Taja jina la samani iliyopo katika picha ambayo hutumiwa kuhifadhia vitabu.

Kabati.

**Kielelezo Na.5.1:** *Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 5*

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliopata alama 0 walishindwa kutambua jina la samani iliyopo katika picha ambayo hutumika kuhifadhia vitabu ambayo ni *kabati*. Wanafunzi hawa walitoa majibu kama vile *ajira, madawati, mlango, meza, maktaba, kuwa pamoja, ofisi ya mwalimu mkuu.* Wanafunzi wengine waliandika vitu visivyoeleweka kama vile *Wanaka, kihoiviarkbe, umochivi na kamtoto.* Wanafunzi walioandika vitu kama *ajira* hawakujua kuwa ajira ni kufanya kazi kwa malipo maalum yanayoitwa ujira au mshahara. Wengine walioandika *madawati* hawakujua kuwa madawati ni kifaa kinachotumika kuandikia au kuhifadhia vitabu au madaftari. Wanafunzi wengine walikosa maarifa kwa kuandika *maktaba* bila kujua kuwa maktaba ni jengo maalum linalotumika kuhifadhia vitabu na machapisho mbalimbali. Walioandika vitu visivyoeleweka wadhihirisha kuwa hawakuwa na stadi za KKK. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi

aliyeshindwa kujibu swali hili. Kielelezo Na.5.3 kinaonesha sampuli ya mwanafunzi aliyeandika majibu yasioeleweka.


**Maswali**

(a) Wanafunzi kwenye hii picha wanafanya nini?

kukusoma pamoja

(b) Unafikiri watoto hawa wapo katika mazingira yapi?

kuchezo pamoja


(c) Ni faida ipi unayoweza kuipata unaposhiriki katika tendo lilioneshwa katika picha?

kukaa a pamoja

(d) Taja jina la samani iliyopo katika picha ambayo hutumiwa kuhifadhia vitabu.

kuyza pamoja

**Kielelezo Na. 5.2:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 5*


**Maswali**

(a) Wanafunzi kwenye hii picha wanafanya nini?

wana ka ana somka

(b) Unafikiri watoto hawa wapo katika mazingira yapi?

wana ka mu ja ana shapeni

(c) Ni faida ipi unayoweza kuipata unaposhiriki katika tendo lilioneshwa katika picha?

wanaka muja ana muja agagna

(d) Taja jina la samani iliyopo katika picha ambayo hutumiwa kuhifadhia vitabu.

wanaka

**Kielelezo Na. 5.3:** *Sampuli ya majibu yasiyoeleweka ya mwanafunzi katika swali la 5*

### 2.2.3 Swali la 6: Kuwa Mwajibikaji


Swali hili liliwataka wanafunzi kusoma kwa umakini kifungu cha habari na kisha kujibu maswali ya kipengele cha (a) – (d) katika nafasi iliyoachwa wazi.

"*Tanzania ni nchi ya amani na utulivu. Amani na utulivu umesababishwa na nchi kuongozwa kwa utawala wa sheria. Sheria hutungwa na Bunge, husimamiwa na serikali na hutafsiriwa na mahakama. Watu wanapaswa kutii sheria na kanuni zinazoongoza nchi.*

*Katika nchi hii, hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria. Wote wanaoshukiwa kuvunja sheria wanapelekwa katika mahakama kujibu mashtaka. Mahakama inapowakuta na hatia hupewa adhabu mbalimbali zikiwemo kulipa faini, kulipa fidia, kifungo gerezani au vyote kwa pamoja.*

*Watu wanaobainika kuvunja sheria hupelekwa mahakamani na kuadhibiwa kwa sababu ukiukwaji wa sheria husababisha ajali, vifo, mlipuko wa magonjwa na migogoro*".

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwajibikaji* na umahiri mahususi wa *Kutii Sheria na Kanuni katika Kutekeleza Majukumu yake ya Kila Siku.* Swali hili lilikuwa na vipengele vinne na kila kipengele kilikuwa na alama 2. Swali lililenga kubaini ufahamu wa wanafunzi wa sheria na kanuni zinazotumika nchini na umuhimu wa kuzifuata katika maisha ya kila siku. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani, ambapo 51.4% ya wanafunzi 1,560,830 walipata alama kuanzia 4 hadi 8. Aidha, 48.6% ya wanafunzi walipata alama kuanzia 0 hadi 2. Kiwango hiki cha ufaulu kimeoneshwa katika Chati Na. 6




**Chati Na.6**: *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 6*

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele:

(a) Nini kinaifanya Tanzania kuwa nchi ya amani na utulivu?

______________________________________________

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kubaini kiini cha nchi ya Tanzania kuwa ya amani na utulivu. Wanafunzi walioelewa kifungu cha habari waliandika majibu sahihi kuwa ni *Kuongozwa kwa utawala wa sheria.* Wanafunzi hao walitambua kuwa sheria ni mfumo wa kanuni ambao hutekelezwa kupitia seti ya taasisi maalumu inayounda siasa, uchumi na jamii kwa njia mbalimbali na huratibu mahusiano baina ya watu. Pia, Wanafunzi hawa walijua kuwa utawala wa sheria unahusisha mfumo wa sheria za nchi ulio wa haki na ambao umejengwa na sheria zisizo kandamizi. Aidha,

husisitiza usawa mbele ya sheria na utendaji wa shughuli za umma kwa pamoja. Katika nchi inayofuata sheria maamuzi lazima yafanyike kwa kufuata sheria za nchi na kuwa na haki sawa mbele ya sheria. Faida za utawala wa sheria ni pamoja na watu wote kuwa sawa mbele ya sheria. Vilevile, haki za raia, wajibu na maslahi hulindwa na mahakama ambapo watu hupewa fursa ya kusikilizwa na ni marufuku mtu kunyang'anywa mali zake.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa kuelewa kifungu cha habari walitoa majibu ambayo si sahihi kama vile; *serikali kutafsiriwa na mahakama, kwasababu tulipata uhuru wetu kisheria, imeongoza kwa utawala mbalimbali, kwa sababu Tanzania inasheria mbalimbali, watu wanajeshi, upendo na mahakamani.* Baadhi ya wanafunzi waliandika vitu visivyo eleweka kwa mfano*; NinikahbikmhlwhkiniMkaiki, mtnikinofnya,* Kwa ujumla, wanafunzi hao walikosa uelewa wa kusoma na kubaini maudhui yaliyopo kwenye kifungu cha habari. Wengine hawakuwa na stadi za KKK ndio maana waliandika mambo yasioeleweka.

(b) Kutokana na habari uliyosoma, kazi ya mahakama ni nini?________________________________________

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kutaja kazi za mahakama. Wanafunzi waliokuwa na uelewa wa kifungu cha habari waliweza kuandika jibu sahihi *kutafsiri sheria/kutoa adhabu kwa wanaobainika kuvunja sheria.* Walielewa kuwa mahakama ni mhimili ambao hutafsiri na kutumia sheria. Aidha, walitambua kuwa mahakama hutoa haki kwa kutatua migogoro. Pia ina wajibu wa kuhakikisha kuwa kuna usawa mbele ya sheria kwa watu wote na mwisho kutumia sheria zilizopo ili kuamua juu ya matumizi hayo. Pia,

mahakama kuu, ina uwezo wa kubatilisha sheria zisizolingana na katiba ya nchi. Mwisho, wanafunzi hawa walielewa kuwa Mahakama, haitungi wala haiundi sheria bali Bunge hufanya kazi hiyo. Walijua pia kwamba kutekeleza sheria ni wajibu wa Serikali. Mahakama hufanya kazi ya kutafsiri na kutekeleza sheria kwa kutafuta ukweli katika kila kesi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi hawakuelewa kifungu cha habari. Hivyo, waliandika majibu mbalimbali ambayo hayakuwa sahihi. kama vile; *kukamata watu, kusimama pale kwenye haki, kuzibiti watu wabaya wauwaji, kupewa adhabu mbalimbali, kazi ya mahakama ni kujibu mashtaka, kazi ya mahakama ni kusimamia nchi, kuwakamata waliofanya makosa, kulipa kifungo gerezani au vyote kwa pamoja.* Wanafunzi wengine waliandika vitu visivyoeleweka kwa mfano; *kukazolanabahesi, kutoAmAFlozo, MahnaksAWAkebtibeiki, n.k.*

Vilevile, majibu yasiyo sahihi ya wanafunzi hawa yanaonesha kuwa walikuwa hawashiriki katika baadhi ya shughuli darasani; kama vile kusoma vifungu vya habari na kuibua maudhui yaliyomo. Wengine wameonesha kukosa stadi za KKK kulikowafanya kuandika vitu visivyoeleweka. Mwisho, wanafunzi hawa hawakuwa na uwezo wa kusoma na kuelewa kifungu cha habari, badala yake walikuwa wanaandika chochote kilichokuwa kinawajia akilini mwao.

(c) Taja adhabu mbili wanazopewa watu wanaobainika kuvunja sheria?

(i) ____________________

(ii) ____________________

Kipengele hiki kiliwataka wanafunzi kutaja adhabu wanazopewa watu wanaobainika kuvunja sheria za nchi. Wanafunzi waliokuwa wamesoma kwa makini kifungu cha habari walibaini jibu sahihi kuwa *ni kulipa faini/kulipa fidia au kifungo gerezani.* Vilevile, wanafunzi hao walielewa kuwa adhabu zitolewazo mahakamani zinalenga kukomesha vitendo visivyofaa katika jamii ambavyo watu hutenda. Wanafunzi walielewa adhabu nyingine zinazotolewa na mahakama kuwa ni hukumu ya kifo na adhabu ya kuchapwa viboko.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wachache hawakuelewa wala kuwa na maarifa ya maudhui kutoka kwenye kifungu cha habari. Hivyo, waliandika majibu mbalimbali ambayo hayakuwa sahihi. Majibu hayo ni kama vile *kusimamiwa na serikali na hatia kupewa, wote wanashukiwa kuvunja sheria, kufagia nyumba, kufungwa, ajali vifo mlipuko wa magonjwa na migogoro, utulivu na amani*, *kuvunja ndoa*, *kupewa taraka, kuvunja sheria, maakama inapowakuta upewa azabu, wanapelekwa katika maakama kujibu sheria.* Aidha, wanafunzi wengine waliacha nafasi bila kuandika chochote na wengine kuandika vitu visivyoeleweka.


(d) Taja athari mbili za ukiukwaji wa sheria.

(i) ______________________________________________

(ii) ______________________________________________

Lengo la kipengele hiki lilikuwa kuwataka wanafunzi kubaini madhara yatokanayo na ukiukwaji wa sheria. Wanafunzi waliokuwa na ufahamu mzuri waliweza kutambua jibu sahihi kuwa ni *kusababisha ajali, vifo, mlipuko wa magonjwa na migogoro*. Wanafunzi hawa waliweza kufahamu maana ya ukiukwaji wa sheria kuwa ni kushindwa au kukataa kufuata sheria yoyote ya nchi

inayotumika. Ni kitendo cha kufanya jambo ambalo haliruhusiwi na sheria au kanuni. Walielewa pia kuwa ukiukwaji wa sheria unaweza kusababisha madhara mengine kama vile; *vitendo vya kikatili dhidi ya raia, matumizi ya nguvu kupita kiasi kwa vyombo vya ulinzi, uharibifu wa mali na uporaji, rushwa na tozo zisizo na viwango maalumu, kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa utendaji, kukamatwa kwa wananchi na kuwekwa kizuizini kinyume na sheria.* Wanafunzi walioandika jibu sahihi walionyesha umahiri wa kusoma kwa ufahamu kwa kuwa waliweza kusoma matini na kuelewa ujumbe uliokusudiwa. Kielelezo Na.6.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi katika swali la 6


**Maswali**

(a) Nini kinaifanya Tanzania kuwa nchi ya amani na utulivu?

nchi kuongozwa kwa utawala wa sheria.

(b) Kutokana na habari uliyosoma, kazi ya mahakama ni nini?

Kazi ya mahakama kutafsiri sheria.

(c) Taja adhabu mbili wanazopewa watu wanaobainika kuvunja sheria.

(i) Kulipa faini.

(ii) Kifungo gerezani.

(d) Taja athari mbili za ukiukwaji wa sheria.


(i) ajali.

(ii) vifo.

**Kielelezo Na 6.1:** *Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 6*

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi hawakuelewa kifungu cha habari kwa kuwa waliandika majibu kama vile, *kifungo gelezani, amani na utulivu umesababishwa na nchi, kuongozwa kwa utawala*

*wa sheria, kujibu mashtaka mahakama, kuwadhibiwa, sheria hutua bunge, mashitaka ya watu, ulalamikaji, na watu wanaovunja sheria.* Lakini pia, baadhi yao waliandika maneno yasioeleweka kama majibu ya maswali walioulizwa. Kwa mfano waliandika: *nbtwywkinithbt, wamasonjwana*, *masya, ayma, ama, musammasamganya, nasamsas, Abtwiywkinatha* n.k. Yaani walishindwa kuandika vizuri. Hii inaonesha uwezo wao mdogo katika kipengele cha kusoma na kuandika kwa ufasaha. Kati yao, wengine hawakuwa na stadi za KKK na hivyo kushindwa kusoma na kuandika majibu yanayoelewaka. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuandika jibu sahihi katika swali hili.


(a) Nini kinaifanya Tanzania kuwa nchi ya amani na utulivu?

imeongoza kwa utawala mbalimbali

(b) Kutokana na habari uliyosoma, kazi ya mahakama ni nini?

watu wanapaswa kutii sheria na kanuni zinazoongozwa

(c) Taja adhabu mbili wanazopewa watu wanaobainika kuvunja sheria.

(i) wanapelekwa katika maakaka kujibu sheria

(ii) maakama inapo wakuta upewa arabu


(d) Taja athari mbili za ukiukwaji wa sheria.

(i) kufungua gelerani wake pamoja

(ii) watu wanao vunja sheria uparekwa maakamani

**Kielelezo Na. 6.2***: Sampuli ya majibuyasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 6*

Aidha, Kielelezo Na. 6.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi alieandika mambo yasiyoeleweka katika swali la 6



(a) Nini kinaifanya Tanzania kuwa nchi ya amani na utulivu?

(b) Kutokana na habari uliyosoma, kazi ya mahakama ni nini?

(c) Taja adhabu mbili wanazopewa watu wanaobainika kuvunja sheria.

(i)

(ii)

(d) Taja athari mbili za ukiukwaji wa sheria.

(i)

(ii)

**Kielelezo Na. 6.3:** *Sampuli ya majibu yasiyoeleweka ya mwanafunzi katika swali la 6*

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Uchambuzi wa umahiri katika maswali ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Uraia na Maadili unaonesha kuwa kati ya aina 6 za umahiri zilizopimwa, aina 3 zimekuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Umahiri huo ni *Kuwa Mwadilifu* katika swali la 1 (76.9%), *Kuwa Mstahimilivu* katika swali la 5 (67.3%) na *Kuithamini Jamii* katika swali la 3 (66.8%). Aidha, umahiri wa *Kuheshimu Jamii* katika swali la 2 (54.8%) na umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* ulikuwa na ufaulu wa wastani. Kwa upande mwingine, umahiri wa *Kudumisha Amani* katika swali la 4 umekuwa na ufaulu hafifu (17%).

Aidha, ulinganifu wa ufaulu wa umahiri kati ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne kwa mwaka 2020 na 2021 unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu cha umahiri wa *Kuwa Mwadilifu* umeongezeka kutoka

ufaulu wa wastani (58.3%) mwaka 2020 kufikia kiwango cha ufaulu kizuri (76.9%) kwa mwaka 2021. Pia, kiwango cha ufaulu cha umahiri wa *Kuheshimu Jamii* kimeshuka kutoka kiwango kizuri cha asilimia 73.1 kwa mwaka 2020 na kufikia kiwango cha wastani wa asilimia 54.8 kwa mwaka 2021. Aidha, ufaulu katika umahiri wa *Kudumisha Amani* umeshuka ubora kutoka kiwango kizuri cha asilimia asilimia 73.6 kwa mwaka 2020 na kuwa kiwango hafifu cha asilimia 17 kwa mwaka 2021. Vilevile, kiwango cha ufaulu katika Umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu* umeendelea kuwa mzuri (68.8%) kwa mwaka 2020 na asilimia 67.3 kwa mwaka 2021. Pia, ufaulu wa umahiri wa *Kuithamini Jamii* ambao nao mwaka 2020 ulikuwa mzuri kwa asilimia 68.2 umeendelea kuwa mzuri kwa asilimia 66.8 kwa mwaka 2021. Mwisho, ufaulu wa umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* ambao haukupimwa mwaka 2020 umekuwa wa kiwango cha wastani cha asilimia 51.4 kwa mwaka 2021. Taarifa zaidi za ufaulu wa wanafunzi zimeambatanishwa katika *Kiambatisho.*

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili umeonesha kuwa, kwa ujumla, wanafunzi wamefaulu kwa kiwango cha wastani hadi kiwango kizuri sana. Daraja A hadi D walikuwa asilimia 91.20, ilhali wachache ambao ni asilimia 8.8 wamepata kiwango hafifu cha ufaulu wa daraja E. Wanafunzi waliofanya vizuri katika upimaji huu walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika umahiri uliopimwa. Aidha waliweza kubaini matakwa ya maswali mbalimbali yaliyoulizwa na pia kumudu vyema stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK).

Kwa upande mwingine, uchambuzi umebaini changamoto mbalimbali za wanafunzi wengine waliokuwa na ufaulu hafifu. Changamoto hizo ni pamoja na kukosa maarifa ya kutosha katika umahiri uliopimwa, kushindwa kujua matakwa ya swali, kukosa stadi za KKK na hivyo kushindwa kuandika sentensi zinazoeleweka. Mwisho, baadhi ya wanafunzi walionesha udhaifu katika kujibu swali la ufahamu kwa usahihi.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi, Baraza la Mitihani linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Walimu waongeze juhudi ya kutumia mbinu mbalimbali katika ufundishaji na ujifunzaji wa umahiri wa *Kudumisha Amani* ambao umekuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Mbinu hizo ni pamoja na:

(i) Matumizi ya igizo dhima ili kuwajengea wanafunzi kumbukumbu ya kudumu kutambua matendo ya kukosa uaminifu.

(ii) Walimu kutumia mbinu ya ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya hadithi fupi kuonesha manufaa ya kuwa mkweli na muwazi.

(iii) Walimu kutumia chati mbalimbali wakati wa kujifunza kuonesha tofauti ya matendo yanayojenga tabia ya kuwa na uaminifu na kukosa uaminifu.

(b) Walimu waandae majaribio na mitihani inayokuza uwezo wa wanafunzi kujibu maswali yanayopima stadi mbalimbali (Kuandika, Kusoma na Kuhesabu).

(c) Wanafunzi wahamasishwe na kuongozwa kusoma vitabu vya kiada na ziada ili kuongeza uelewa wao wa umahiri mbalimbali wa somo hili.

(d) Walimu wawahusishe wanafunzi katika upimaji ambao unaweza kufanyika baada ya mchakato wa ufundishaji na uijfunzaji wa kawaida nje ya darasa ili kuimarisha uelewa wa wanafunzi kwa vitendo

*Kiambatisho*

**Ulinganifu wa ufaulu kwa wanafunzi katika kila umahiri kwa mwaka 2020 na 2021**

| | **Umahiri** | **UPIMAJI 2020** | | | | **UPIMAJI 2021** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Ufaulu wa kila swali** | | **Wastani wa ufaulu (%)** | **Maoni** | **Ufaulu wa kila swali** | | **Wastani wa ufaulu (%)** | **Maoni** |
| | | **Namba ya swali** | **% wa ufaulu** | | | **Namba ya swali** | **% wa ufaulu** | | |
| 1 | Kuwa Mwadilifu | 3 | 58.3 | 58.3 | Wastani | 1 | 76.9 | 76.9 | Vizuri |
| 2 | Kuwa Mstahimilivu | 2 | 68.8 | 68.8 | Vizuri | 5 | 67.3 | 67.3 | Vizuri |
| 3 | Kuithamini Jamii | 5 | 68.2 | 68.2 | Vizuri | 3 | 66.8 | 66.8 | Vizuri |
| 4 | Kuheshimu Jamii | 4 | 73.1 | 73.1 | Vizuri | 2 | 54.8 | 54.8 | Wastani |
| 5 | Kuwa Mwajibikaji | | | | | 6 | 51.4 | 51.4 | Wastani |
| 6 | Kudumisha Amani | 1 | 73.6 | 73.6 | Vizuri | 4 | 17 | 17 | Hafifu |